

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

11/04/2019

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA ATIMIZA AHADI YA KUWAPATIA WAJANE MILIONI 10 NA KUWAJENGEA JENGO LA MAKAO MAKUU YA CHAMA CHA WAJANE TANZANIA.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo ametimiza ahadi yake aliyoitoa juzi ya kuwapatia wajane kiasi cha Shilingi milioni 10 za kusaidia kutatua changamoto za kiofisi zilizokuwa zikiwanyima usingizi wajane ikiwemo ya malimbikizo ya madeni ya kodi kwenye nyumba wanayoitumia kama ofisi.

Itakumbukwe kuwa wakati wa kongamano la wajane RC Makonda alitoa ahadi ya kuwapatia milioni 10 na kuwatafutia eneo la kujenga jengo la ofisi za makao makuu ya chama cha wajane Tanzania na tayari eneo limepatikana tayari kwa ujenzi.

Mapema Leo Afisa elimu wa Mkoa wa Dar es salaam Hamis Lissu amewakabidhi milioni 10 kwa niaba ya RC Makonda ambae yupo katika majukumu mengine ya kitaifa.

Kwa upande wao wajane wamemshukuru RC Makonda kwa kuwasaidia kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili na wanaamini kupitia uongozi thabiti wa RC Makonda ujenzi wa jengo la makao makuu ya chama hicho utakamilika kwa uharaka.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

